JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA

SHULE YA SEKONDARI PAMBA

Simu: +255 28 2502721
+ 255 0767 492956

S.L.P. 632,
MWANZA

1.0: **UTANGULIZI:**

Ninayo furaha kubwa kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Pamba mwaka wa masomo 2021. Shule ya Sekondari Pamba ni shule ya Kutwa ambayo ipo umbali wa km. 3 kaskazini/magharibi/kusini mji mkuu wa Mkoa/Halmashauri ya Jiji la Mwanza. Usafiri unaotumika ni wa daladala (mabasi madogo yanayofanya safari zake ndani/katikati ya jiji la Mwanza. Nauli inayotozwa kwa mwanafunzi kutoka kituo kimoja hadi kingine ni Tshs. 200/= kwa mwanafunzi. Shule itafunguliwa Januari **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **25/01/2021**. Mara baada ya wanafunzi kufungua shule tarehe 11/01/2021 na kufanyiwa usajili wanafunzi wote wataanza kusoma ("Orientation Course") kwa kipindi cha wiki nane hivyo unashauriwa kuhakikisha kuwa mwanao anaripoti shuleni kwa wakati bila kukosa ili aweze kuhudhuria mafunzo hayo muhimu.
Karibu sana Pamba Sekondari.

2.0: **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**:

2.1: Sare za shule

(a) Sare ya shule hii kwa wavulana:-
1. Suruali nyeusi (2) na Shati nyeupe 2 mikono mifupi

(b) Sare ya Wasichana:-
1. Sketi dark bluu (2) na shati nyeupe 2 mikono mifupi
- ❖ Mashono yameambatanishwa pamoja na rangi za vitambaa husika.

(c) Rangi ya Hijab pamoja na mashono (njoo uangalie sample shuleni)

(d) Sare ya michezo kwa shule hii ni Bukta, T.shirt na raba (rangi yoyote) kwa wasichana na wavulana.

2.2: Daftari (zisizopungua 10) kalamu na mkebe wa hesabu

2.3: Chakula cha mwanafunzi wa kutwa, nauli ya kwenda na kurudi nyumbani pamoja na matibabu.

3.0: Sheria na Kanuni muhimu za shule hii:-

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Ofisi ya Rais TAMISEMI.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
(d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
(f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
(g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
(h) Kutunza mali za umma.

3.2: **MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUKUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE:**

(a) Wizi
(b) Uasherati
(c) Ubakaji
(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika
(e) Kupigana au kupiga
(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
(g) Kudharau bendera ya Taifa
(h) Kuwa mjamzito/kupata mimba
(i) Kutoa mimba
(j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
(k) Kukataa adhabu kwa makusudi
(l) Kuwa na simu ya mkononi.

4.0: **MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI:**

(a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga wa hosptali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni. (Nyongeza D)
(b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. (nyongeza C)
(c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatayotolewa na shule. (Nyongeza B)

5.0: ***Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza Kikamilifu.***

HONGERA NA KARIBU SANA PAMBA SEKONDARI!!

.....

MKUU WA SHULE

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA
SHULE YA SEKONDARI PAMBA

SHERIA ZA SHULE

1. Hairuhusiwi mwanafunzi kuvuta bangi kunywa pombe au kutumia madawa yoyote ya kulevya. Hili ni kosa la kufukuzwa shule.

2. Ni kosa kuchelewa kufika shule kwa wakati.

3. Hairuhusiwi kufanya mgomo, kuchochea kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au wa watu. Hili ni kosa la kufukwa shule.

4. Mwanafunzi haruhusiwi kujiunga na makundi ya wahuni. Akigundulika hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.

5. Ni marufuku mwanafunzi kujihusisha na tabia ya Uasherati, Ushoga, Ubakaji na Usagaji. Hili ni kosa la kufukuzwa shule.

6. Wizi wa aina yoyote hauruhusiwi shuleni na nje ya shule. Hili ni kosa la kufukuzwa shule.

7. Kupigana au kutishia kupigana ndani au nje ya shule na kutumia lugha chafu (matusi) ni marufuku. Ikithibitika kuwa umeshiriki utafukuzwa shule.

8. Hairuhusiwi mwanafunzi kuharibu mali ya umma. Ukifanya hivyo utalipa fidia ya uharibifu.

10. Ni kosa kwa mwanafunzi kukataa adhabu kwa makusudi

11. Hairuhusiwi mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi. Ukikamatwa na simu itaharibiwa/itavunjwa hadharani.

12. Ni kosa mwanafunzi kutovaa vazi rasmi la shule mf. Mlegezo, kutovaa tai, nembo na sketi fupi n.k. Ukionekana adhabu kali itatolewa dhidi yako.

13. Ni kosa mwanafunzi kuwa na mimba/kutoa mimba, kusababisha mimba. Hili ni kosa la kufukwa shule.

14. Mwanafunzi haruhusiwi kuingia nyumba za starehe (clubs, guest house)

15. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi kunyoa mitindo ya kihuni au kusuka nywele.
16. Utoro wa makusudi utasababisha wewe kufukuzwa shule.

NYONGEZA "B"

SHULE YA SEKONDARI PAMBA

HATI YA KUKUBALI KUINGIA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

- Mimi (Jina la Mwanafunzi).....nimepokea barua ya masharti ya kujiunga na shule ya Sekondari Pamba. Naahidi kutii amri zote halali zitakazotolewa na walimu na walezi wangu wengine shuleni.
- Nitafanya kazi zozote zitakazoiletea shule yangu na Taifa sifa nzuri, maendeleo na heshima.
- Nitafanya jitihada katika masomo yangu wakati wote.
- Naelewa kwamba wakati wote nitakapokuwa mwanafunzi nikifanya makosa yafuatayo nitafukuzwa shule.

1. Kuvuta bangi/ kunywa pombe au kutumia Madawa yoyote ya kulevya
2. Kuchelewa kufika shule/utoro
3. Kufanya mgomo, Kuchochea, Kuongoza au Kuvuruga amani na Usalama wa shule au wa watu.
4. Kujiunga na makundi ya wahuni
5. Kudharau Bendera ya Taifa
6. Kupatikana na mimba/kutoa mimba/kusababisha mimba (wavulana) ndani na nje ya shule.
7. Uasherati na Ushoga
8. Wizi
9. Kupigana au kutishia kupigana ndani au nje ya shule na kutumia lugha chafu (matusi)
10. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
11. Kukataa adhabu kwa makusudi/kugomea adhabu itolewayo shuleni
12. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi
13. Kutovaa vazi rasmi la shule mf. Mlegezo, kutovaa Tai, Nembo na Sketi fupi.

Saini ya mwanafunzi .....
Anuani
.....

SAINI NA UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI

Mimi..... ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi ..... nakubaliana na masharti yote ya shule kama yalivyoainishwa hapo juu na ninaahidi kutoa ushirikiano kwa shule pale nitakapohitajika.

Saini ..... Tarehe .....

NYONGEZA "C"

HISTORIA YA MWANAFUNZI

1. Jina lako: .....
   (Jina hili ni lazima libaki hivi hivi kwa miaka ijayo
   Utakapokuwa shuleni)

Picha ya Mwanafun



2. **BABA**:
   (a) Jina la Baba yako ni : .....
   (b) Yu hai amefariki : .....
   (c) Kama amefariki lini : .....
   (d) Anuani yake : .....
   (e) Kazi na cheo chake: .....
   (f) Dini ya Baba yako ni: .....
   (g) Namba ya Simu: .....

Picha ya Baba



3. **MAMA**:
   (a) Jina la Mama yako .....
   (b) Yu hai au amefariki .....
   (c) Kama amefariki lini .....
   (d) Anuani yake /cheo chake .....
   (e) Namba ya simu .....

Picha ya Mama

4. Mlezi (i) Unaye mlezi ? Mlezi ni mtu asiye mzazi wako anayekutunza na kuhudumia kwa Chakula, Malazi n.k. NDIYO/HAPANA .....



   (a) Jina la Mlezi huyu ni .....
   (b) Uhusiano wako na Mlezi ni (Mjomba, Kaka, Rafiki, Shangazi (n.k).....
   (c) Anuani ya melzi wako ni .....
   (d) Kazi ya mlezi wako ni .....
   (e) Namba yake ya Simu .....

Picha ya Mlezi

5. (i) Jina la mtu atakayepelekewa ripoti zako za shule kama Baba/Mama au Mlezi wako ni .....
   Anuani yake ni .....
   Sahihi ..... Tarehe .....
   Namba ya Simu .....

   SAHIHI YA MWANAFUNZI: .....
   SAHIHI YA MZAZI/MLEZI: .....
   JINA LA MZAZI/MLEZI: .....

NYONGEZA "D"

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA

TAARIFA YA MWANAFUNZI KUTOKA ENEO ANALOTOKA

1. **Taarifa ya mtendaji wa mtaa mwanafunzi anakoishi**

- Jina.....Sahihi.....
- Namba Ya Simu .....

2. **Taarifa ya mwenyekiti wa mtaa mwanafunzi anakoishi**
   - Jina .....Sahihi.....
   - Namba Ya Simu.....

3. **Taarifa ya mtendaji wa kata mwanafunzi anakotoka**

- Jina .....Sahihi.....
- Namba Ya Simu.....

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANA
MINISTRY OF EDUCATION SCIENCE & TECHNOLOGY
PAMBA SECONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM

TO BE COMPLETED BY THE MEDICAL OFFICER IN RESPECT TO ALL FORM "I" ENTRANTS

PUPIL'S FULL NAME .....

AGE ..... SEX .....

STOOL EXAMINATION .....

BLOO DCOUNT (RED AND WHITE) .....

URINALYSIS .....

SYMPHLIS TEST .....

EYE TEST .....

CHEST .....

SPLEEN .....

ADDITIONAL INFORMATION (E.G Physical defects/impairment or chronic disease requiring special treatment/attention) .....

I certify that I have examined the above pupil and recommend that he/she is fit/unfit to pursue Secondary Education.

Signed .....

Designation .....

DATE: ..... OFFICIAL STAMP .....

(Delete whichever is in applicable)

UNIFORM (SKETI)



RANGI YA DARK BLUE

Utepe mweupe mbele (mistari miwili)

Marinda madogo madogo

NB: Mfuko wa sketi uwe na zipu nyeusi au dark blue.

Shati la mikono mifupi la rangi nyeupe.

Aweke bar (I) nyeusi begani kuonesha kidato cha kwanza.
Tai ya **dark blue** ifanane na rangi ya sketi.

UREFU WA SKETI NI SENTIMITA 15 KUTOKA MAGOTINI

UNIFORM (SURUALI)



- **RANGI: Nyeusi.**
- **Iwe na mfuko mmoja wa nyuma.**
- **Shati la mikono mifupi jeupe na tai NYEUSI.**
- **Sweta la dark blue.**
- **Aweke bar (I) kuonesha kidato cha kwanza.**

UNIFORM (HIJAB)



NB: Aweke bar (I) begani kuonesha kidato cha kwanza.
Viatu vyenye kisigino kifupi vya ngozi nya kufunga na kamba.